TOLEO NO. 01
SEPTEMBA, 2025

SELF MICROFINANCE FUND

SELF MF

"Kuwapa Watu Fursa ya Kufanya Shughuli za Uzalishaji Mali"

JARIDA HILI HALIUZWI

TULIPOTOKA, TULIPO NA TUNAPOELEKEA UTEKELEZAJI DIRA YA TAIFA - 2050

JINSI MIKOPO NAFUU INAVYOWANASUA WANANCHI KUTOKA JANGA LA UMASKINI

BODI YA MFUKO WA SELF WATEMBELEA WANUFAIKA-ARUSHA

NITATUMIA UWEZO WOTE KUCHOCHEA UFANISI MFUKO WA SELF-SANGAWE

AFYA & MAZINGIRA: MIKOPO NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUWAFIKIA WENGI

SALAMU YA MWENYEKITI WA BODI

"SAFARI KUFIKIA MALENGO DIRA YA TAIFA, TUMEJIPANGA VEMA"

PAUL SANGAWE
Mwenyekiti wa Bodi- SELF Microfinance

Kwa niaba ya Bodi ya SELF Microfinance Fund, ndugu msomaji wetu, ninayo furaha kubwa kukukaribisha, kupata elimu kwa habari na makala za kina kuhusu Mfuko wetu.

Jarida hili la kwanza ni maalum ambalo limebeba taarifa nyingi muhimu ambazo kwa kina zinaeleza wapi tulipotoka, wapi tulipo na wapi tunapoelekea katika kuitumikia jamii yetu. Mfuko wa SELF ni taasisi iliyo chini ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha ambao ulianzishwa mnamo mwaka 2015 kwa lengo la kuwezesha wananchi kukua kiuchumi.

Tuna wajibika kutoa mikopo nafuu kwa wajasiriamali wadogo, kusaidia taasisi ndogo za ki-fedha (microfinance] ambazo zimejikita kusaidia wananchi katika ngazi ya chini kabisa kwenye jamii. Hasa kwa wananchi wale ambao hawana uwezo wa kupata dhamana kubwa kukopa kwenye mabenki mbalimbali ili kukuza biashara zao na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

Nisimalize uhondo wote juu ya yale ambayo yameandikwa kwa ustadi mkubwa kukujuza kiundani, nitumie ukurasa huu pia kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliotufikisha hapa tulipo. Safari yetu imekuwa ya kujituma, kushirikiana na kuleta matokeo chanya yanayoonekana katika maisha ya maelfu ya Watanzania.

Ni fahari kwetu kuona wananchi zaidi ya 183,000 wamenufaika na mikopo nafuu na ajira mpya zaidi ya 183,000 zikiibuka kutokana na uwezeshaji huu kuanzian 2021 hadi 2025. Kupitia jitihada hizi.SELF Microfinance Fund tumejidhihirisha kama nyenzo madhubuti ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mwelekeo wetu wa miaka ijayo ni kuhakikisha huduma za kifedha zinabaki kuwa jumuishi, za kidigitali na zenye kugusa sekta zote muhimu ikiwemo afya na mazingira. Bodi itaendelea kusimamia kwa karibu kuhakikisha tunabaki mstari wa mbele katika kuchochea maendeleo ya Taifa letu, karibu sana.

PAUL SANGAWE

Mwenyekiti wa Bodi - SELF Microfinance

SALAMU YA AFISA MTENDAJI MKUU

"UWEZESHAJI WA KI-FEDHA KWA KILA MTANZANIA"

SANTIELI YONA

Afisa Mtendaji Mkuu-SELF Microfinance Fund

Ndugu Msomaji wetu, ni heshima kuwasilisha salamu hii kwa kukubali kusoma jarida ili kujifunza na kupata elimu kuhusu SELF Microfinance Fund, huduma zetu mbalimbali tulizonazo. Tumepata mafanikio kadhaa ikiwamo katika kipindi cha miaka minne (2021–2025), Mfuko wa SELF tumeona ukipiga hatua kubwa katika kuihudumia jamii, nchini Tanzania.

Tumeweza kutoa mikopo yenye thamani ya TZS 196.9 Bil. na kuwafikia wanufaika zaidi ya 183,000 pia tumetengeneza faida ya TZS 4.73 Bil. huu ni ushahidi wa uthabiti wa ki-utendaji wa taasisi yetu, tumeweza pia kuchangia katika kuzalisha ajira ikiwamo za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Tunajivunia pia hatua tulizopiga katika kuongeza matawi kutoka 8 hadi 12, sambamba na kuimarisha mifumo ya kidigitali ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

Tukiwa tunaelekea mwaka 2030, mpango wetu wa kufanikisha mikopo ya thamani ya TZS 300 Bil. kwa zaidi ya wananchi 200,000 ni ushahidi wa dhamira yetu ya kweli. Tunatambua kuwa maendeleo ya kifedha hayawezi kutenganishwa na afya bora pamoja na mazingira endelevu, ndiyo maana tunapanua huduma zetu hadi katika sekta za nishati safi ya kupikia na miradi ya kijamii.

Kwa pamoja, tunaweza kuijenga Tanzania yenye uchumi jumuishi na mustakabali bora kwa vizazi vijavyo, karibu.

SANTIELI YONA

Afisa Mtendaji Mkuu - SELF MicrofinanceFund

TAHARIRI

TUMEDHAMIRIA KUJENGA TANZANIA YENYE UCHUMI JUMUISHI

LINDA MSHANA

Meneja Masoko na Uhamasishaji-SELF MicrofinanceFund

NDUGU Msomaji wetu, hili ni jarida letu maalum na la kwanza kwa SELF Microfinance Fund, hatua hii muhimu inalenga kupanua wigo wa uelimishaji jamii kuhusu huduma tunazotoa katika uwezeshaji wananchi ki-uchumi kwa mikopo nafuu, pamoja na elimu ya biashara.

Ninapenda kutumia nafasi hii kukukaribisha kusoma habari pamoja na makala tulizokuandalia pia utapata simulizi za moja kwa moja kwa baadhi ya watu walionufaika na huduma zetu za Mfuko namna ambavyo mikopo nafuu imeweza kuinua kiwango chao cha mitaji na kukua ki-uchumi.

Aidha, tumeeleza vema namna ambavyo SELF Microfinance Fund tumejipanga kuitekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo inatutaka kila taasisi kuwajibika kwa kuangalia nafasi yake katika safari hiyo. Kwa mantiki tumeeleza vile ambavyo tutaendelea kuwa chachu ya mageuzi ya kifedha nchini, tukiwaleta wananchi wa kipato cha chini na wa kati karibu na fursa za ki-fedha zenye masharti nafuu.

Jarida hili, linadadavua kwa kina zaidi, kwa takwimu pamoja shuhuda halisi, kutoka kwa wanufaika wetu, tunapenda ujifunze zaidi namna huduma zetu za ki-fedha zilivyojikita kwa jamii na zinavyoleta mabadiliko makubwa ya ki-jamii na ki-uchumi.

Kadri tunavyoelekea mwaka 2030 na hatimaye 2050, tumejipanga vema kuendelea kuwa mshirika wa kweli wa maendeleo ya wananchi, si tu kwa kutoa mikopo nafuu, bali pia kupitia elimu ya ki-fedha, uendelevu wa mazingira na afya bora ya jamii na huduma za bima mbalimbali. Jarida hili ni kioo cha safari hiyo ni mwaliko kwa kila mmoja kushiriki katika kujenga mustakabali wa Taifa letu, tumedhamiria kujenga Tanzania yenye uchumi jumuishi kwa pamoja, karibu sana .

LINDA MSHANA

Meneja Masoko na Uhamasishaji - SELF MicrofinanceFund

TULIPOTOKA, TULIPO NA TUNAPOELEKEA UTEKELEZAJI DIRA YA TAIFA - 2050

Huduma za ki-fedha ni mojawapo ya kichocheo muhimu cha mageuzi ya ki-uchumi Tanzania kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 – 2050.

Kwa kuzingatia fursa zilizopo SELF Microfinance Fund [Mfuko wa SELF] umebainisha vipaumbele vinane itakayosimamia madhubuti ili kufikia malengo ya Dira hiyo ya Taifa.

Dira hiyo ilizinduliwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Julai 17, 2025 ndani ya Jiji la Dodoma.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa SELF Paul Sangawe anasema wameona vema kujipanga upya katika utekelezaji wa majukumu yao kufikia lengo.

Sangawe anasisitiza "Ni muda mwafaka wa kila taasisi kujipanga vema kuona namna gani itaweka mipango yake ili iendane na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050".

Anasema uzinduzi wa Dira hiyo tafsiri yake mojawapo ni pamoja na mashirika, taasisi za umma kujipanga upya kwa kuzingatia malengo na vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika Dira.

"Kwa hiyo pamoja na mafanikio ambayo tumepata, tunadhani huu ndiyo muda wa kujipanga, kufanya jitihada ili kuhakikisha mfuko unaendelea kuhudumia wananchi kwa ufanisi,".

Anaongeza "Lakini pia vile vile, kufikia malengo na vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika dira.

"Katika kipindi kijacho [2025 2030] mfuko utatoa vipaumbele katika maeneo makubwa yafuatayo,

"Tumejipanga kuandaa mpango wa muda mrefu utakaotafsiri 'vision' ya Dira ya Taifa, tunataka tuwe na mpango wa muda mrefu utakaoendana na mipango ya ki-Taifa na Kimataifa,".

Anaongeza "Tunajua tunaenda kwenye Uchaguzi Mkuu, kuna chama ambacho kitashinda kwa hiyo kutakuwa na ilani ambayo itakuwa inatekelezwa.

"Ndiyo maana tunaandaa sasa mipango itakayolenga kuongeza mtaji ili kuwafikia wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huduma za Mfuko huu," anasisitiza.

Sangawe anafafanua "Nimesema tuna mtaji sawa lakini watanzania ni wengi na population idadi ya watu inaongezeka, wenye mahitaji wanaongezeka.

"[Hivyo] 'focus area' ya pili, eneo la kimkakati ni kuongeza mtaji wa Mfuko ili tuweze kuhudumia wengi kadri inavyowezekana," anabainisha.

Anasema pia wanalenga kupanua wigo wa huduma kwa kuongeza idadi ya matawi waliyonayo kwani ya sasa ambayo ni 12 bado hayatoshi.

"Kwa hiyo tunakwenda kufanya uchambuzi kuona kimkakati tumejipangaje kwenda awamu kwa awamu kuongeza matawi katika mikoa mingine ambayo imebaki ili wananchi wasipate shida kutafuta tulipo,".

Anasisitiza "Wakitafuta waipate kwa urahisi na huduma wanayohitaji waweze kuipata bila kutumia muda mrefu.

"Pia tutaimarisha ushirikiano, tunajua hatupo wenyewe sokoni kuna taasisi nyingi za fedha nyingine ni kubwa, nyingine ni ndogo.

"Tutakwenda kuimarisha ushirikiano na tumeshaanza tayari, pia na wadau wa maendeleo wa ndani ya nchi na nje ya nchi ," anasema.

Sangawe anasema hatua hiyo inalenga kukuza utoaji wa huduma zao lakini pia kujiimarisha, katika kuongeza mtaji sambamba na uwezo wa mfuko katika kuhudumia wateja.

"Tunajua kwenye mkopo jambo ambalo linakimbiza wengi ni 'issue' ya riba, hili ni tatizo kubwa," anasema.

"Lakini Mfuko kwenye eneo hili nalo tunaenda kufanya uchambuzi kuhakikisha tunakuwa na riba rafiki kwa watumiaji.

"Tusije tukazungumza suala la wananchi kuumizwa katika taasisi nyingine ndogo ndogo za mikopo na SELF iwe mmoja wao hapana," anasema.

"Tutaangalia kwa upya katika eneo la riba kuhakikisha zinakuwa rafiki na wananchi wananufaika na si wanaumizwa na riba,".

Anasema pia wataendelea kuelimisha wananchi vile vile kutangaza huduma za mfuko ili kuongeza wigo, tunajua SELF haifahamiki nchini kote na Tanzania ni kubwa.

"..., na ili kuongeza huduma na kutoa huduma ni pamoja na kuongeza kujulikana, hivyo eneo ambalo tutalizingatia pia ni kuongeza 'visibility'.

Anasema pia wanalenga kuboresha na kurahisisha utoaji wa huduma, matumizi ya teknolojia ili wananchi wapate huduma kwa urahisi zaidi.

"Wale wanaoweza kutumia teknolojia 'ku-apply' mikopo na kufanyiwa 'assessment online' na kupata mikopo hiyo kwa wakati.

Anasema wanataka kuendelea kutoa gawio kwa Serikali kwa sababu watakuwa wameweza kuongeza mtaji na faida.

"Tuwe na mchango katika maendeleo ya Taifa, kama SELF mchango wetu uendelee kukua na kuongezeka kadri itakavyokuwa ambavyo mtaji wa taasisi utaendelea kukua.

"Tunafanya kazi na hii ni taasisi kubwa tutaendelea kuimarisha ushirikiano wa wafanyakazi, bodi na wateja," anasema.

Sangawe anasisitiza "Tukiweza kufanya yote haya tutakwenda kufikia malengo ya Mfuko wa SELF.

UCHUMI: WATU 180,000+ WANUFAIKA MIKOPO NAFUU KUKUZA BIASHARA

Uchumi wa watu zaidi ya 180,000 umesaidiwa kwa kupata mikopo nafuu kwa ajili ya kukuza biashara zao na shughuli nyingine za kujipatia kipato, nchini Tanzania.

Idadi hiyo ya watu ni wale waliohudumiwa na SELF Microfinance Fund ndani ya kipindi cha 2020/21 hadi Juni, 2025 pekee.

Ni mfuko unaomilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa 100% ukiwa chini ya Wizara ya Fedha ulioanzishwa mnamo mwaka 2015 kwa lengo la kusaidia wananchi kupata mikopo nafuu.

Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona akizungumza na waandishi wa habari pamoja na wahariri katika Mkoa wa Dar es Salaam, amebainisha hayo.

"Mikopo hiyo imesaidia hasa wanawake na vijana kuanzisha biashara na kuongeza kipato," amesema.

Ametaja mfano halisi, ni mwanamke mmoja aishiye Dar es Salaam ambaye anajishughulisha na ufugaji, ni mmoja wa wanufaika wa mfuko huo.

"Alianza na ng'ombe wanne tu, lakini kwa sasa anafuga ng'ombe zaidi ya 24 pamoja na mbuzi na nguruwe.

"Hii inaonesha mikopo ikitumika vizuri inaweza kubadilisha maisha," amesema Santieli na kuongeza,

"SELF Microfinance Fund imekuwa ikitoa pia elimu ya fedha kwa wananchi, tunawafundisha namna ya kufanya tathmini ya miradi yao kabla ya kuchukua mikopo ili watimize malengo.

Mfuko wa SELF unahudumia wananchi kote nchini, lakini hivi sasa umeweza kuwa na matawi 12 yaliyosambaa sehemu mbalimbali nchini.

Lengo ni kuongeza idadi hadi 22 miaka mitano ijayo na wana dhamira kufungua matawi katika kila mkoa kwa miaka ya mbele.

Hatua hii inalenga kupanua wigo wa huduma zetu na kufikia wananchi wengi ili wanufaike na mikopo kutoka SELF Microfinance Fund.

"NITATUMIA UWEZO WOTE, KUCHOCHEA UFANISI MFUKO WA SELF"- SANGAWE

Jukumu kubwa alilopewa kuongoza tena Bodi ya SELF Microfinance Fund, Paul Sangawe ameahidi atalitekeleza kwa uwezo wake wote aliojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa ushirikiano na wafanyakazi wa Mfuko huo, wadau wa maendeleo wa ndani na nje pamoja na wateja ambao wanaowapatia huduma atahakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea.

Mfuko wa SELF ni kati ya taasisi zilizo chini ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ambayo ina jukumu la kutoa elimu ya fedha pamoja na mikopo nafuu kwa wananchi.

Sangawe ameongoza kikao cha kwanza cha wajumbe wa bodi hiyo ili kuweka mikakati ya pamoja ya utekelezaji wa majukumu yao kwa miaka mingine mitano ijayo.

"Nimeona vema kukutana nanyi waandishi wa habari ikiwa ni sehemu ya kutekeleza majukumu ya msingi ya SELF Microfinance Fund, kutoa taarifa kwa wananchi na wateja tunaowahudumia.

"Namshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua tena kuongoza bodi hii ya Mfuko wa SELF kwa kipindi cha pili.

Ameongeza "Kwa sababu Watanzania wenye uwezo ni wengi, lakini imempendeza kuniteua kuhudumu tena, namshukuru sana.

"Naahidi nitatumia uwezo wangu wote kuhakikisha majukumu niliyopewa tutaendelea kuyatekeleza kwa ufanisi wa hali ya juu," amesisitiza.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti huyo wa Bodi, Afisa Mtendaji Mkuu Santieli Yona amesema kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 wamepata mafanikio.

Amesema jukumu kubwa la kwanza ambalo Mfuko huo unawajibika kulitekeleza ni kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kuinuka ki-uchumi.

Jukumu jingine ni kutoa mikopo kwa taasisi za fedha zinazolenga kutoa huduma za ki-fedha kwa wananchi katika ngazi ya chini kabisa ya jamii.

"Tangu 2015 hadi sasa, tumefanikiwa kutoa mikopo zaidi ya TZS 397 Bil, wamenufaika watu 246,401 wanawake ni 53% kati ya hao," amesema.

UFANISI, WIGO HUDUMA ZA MFUKO WA SELF KUPANULIWA-KI-DIGITALI

Wigo wa huduma za mikopo nafuu utaongezwa zaidi ndani ya SELF Microfinance Fund ikiwamo kuongezwa idadi ya matawi yake kutoka 12 ya sasa hadi 22.

Ongezeko hilo linatarajiwa ndani ya miaka mitano ijayo [2025 – 2030] lengo ni kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na kunufaika.

Yameelezwa hayo na Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona mbele ya waandishi wa habari na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ndani ya Dar es Salaam.

"Jinsi tulivyojipanga [ni kufikia] kila tawi linakuwa na mikoa ambayo inatoa huduma. Nia yetu baadae ni kufungua matawi mengi zaidi, tutakwenda nchi nzima," amesema.

Amesema wamelenga kuimarisha mifumo yake ki-digitali ili kwenda sambamba na kasi ya ukuaji na mabadiliko ya ki-teknolojia katika utoaji na ufikiwaji wa huduma za ki-fedha nchini.

"SELF Microfinance Fund imejikita pia kwenye utoaji wa elimu ya fedha, bima za kulinda mikopo na usaidizi kwa taasisi ndogo za kifedha nchini," amesema.



FAIDA: NDANI YA MIAKA 4 ZIMEPATIKANA TZS BILIONI 4.73- ILLOMO

Uelekeo wa Serikali ya Tanzania kwa mashirika yake ya Umma ni lazima yajisimamie na kujitegemea ki-uchumi, bila kutegemea Serikali Kuu.

Agizo ambalo SELF Microfinance Fund imemudu kulitekeleza ndani ya kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2020/21 hadi Juni, 2025.

Kwa uthabiti mfuko huo umeendelea kuwezesha wananchi ki-uchumi kwa kuwapa mikopo nafuu huku pia ikiweza kutengeneza faida ya kiasi cha TZS 4.73 Bil. ndani ya kipindi hicho.

Ni mfuko ulio chini ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ambapo hufanya shughuli zake kwa uthabiti na ufanisi.
"SELF Microfinance Fund umezingatia maelekezo ya Serikali," amesema Mkurugenzi wa Huduma za Shirika SELF Microfinance Fund Christopher Illomo.

Ni katika mkutano wa SELF Microfinance Fund na waandishi wa habari pamoja na wahariri wa vyombo mbalimbali ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.
Illomo ameongeza "Rais Samia aliyataka mashirika ya Umma kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu, kwamba yajiendeshe yenyewe na sisi tumeweza kujiendesha.

"Tunaweza kufanya biashara kwa huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo, tunajilipa mishahara na gharama zingine za uendeshaji," amebainisha.
Amesema kwa hatua hiyo wameweza kulipa kodi zote stahiki zinazotakiwa vile vile kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi Juni, 2025 wametengeneza faida hiyo ya TZS 4.73 Bil.

"Katika faida hiyo tumetoa gawio kwa Serikali 15% ya hiyo faida," amesema na kuongeza, "Kwa hiyo Serikali imehakikisha tunaweza kurudisha hiyo faida kuwapa huduma wananchi na kutoa gawio hilo,".

Awali, Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona amesema wamejidhatiti kupanua wigo zaidi wa huduma zao kwa jami, ndani ya miaka mitano ijayo.

UKUAJI WENYE TIJA, AJIRA & UCHUMI KWA THAMANI YA TZS BILIONI 196.9

Upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu ili kusaidia wananchi kukuza biashara zao na vipato vyao ni eneo la kwanza linalosimamiwa na SELF Microfinance Fund.

Ndani ya kipindi cha miaka 4 [yaani mwaka 2020/21 hadi Juni, 2025] mfuko huo unajivunia kufikia lengo hilo, madhubuti.

"[Kwa kipindi hicho] tumeweza kutoa mikopo yenye thamani ya TZS 196.9 Bil na katika utoaji wa mikopo hii katika kitu tunazingatia sana ni ubora wa ile mikopo,".

Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona amesema hayo alipozungumza na waandishi wa habari pamoja na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari, Dar es Salaam.

Ni katika vikao endelevu vinavyoandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa lengo la kuhakikisha taasisi zilizo chini yake zinaeleza Umma majukumu yake na namna zinavyowahudumia.

Santieli ameongeza "Wakati mwingine inapimwa na kitu fulani wanasema kiwango cha mikopo chechefu.

"Kwa kweli katika kipindi hicho tumeweza kuhakikisha kiwango cha mikopo chechefu yetu hakizidi 10%. Kwa hiyo tumekuwa chini ya 10% ambazo wakati mwingine imekuwa 8%.

"Hii inaonesha nini? [ni] kwamba hii mikopo ambayo tunaitoa inarudi kwa hiyo ndiyo maana kama ni mtaji wa serikali unaweza kuzunguka na mwishoni tukazalisha zaidi.

"Lakini muhimu zaidi katika kutoa hii mikopo ambayo nimeitaja katika vipindi vyote tangu 2020/21 hadi sasa tunajiendesha kwa faida," amebainisha.

Amefafanua zaidi, "Hii kwetu sisi ni fahari kwa sababu tunatambua huu ni uwekezaji mkubwa ambao Serikali imeweka na inatamani twende kwa wananchi, tuwafikie.

"Kwa hiyo mwisho wa siku lazima tuwe na faida na tukiwa na faida inaonesha nini?... [ni] kwamba tutaendelea kuwepo na kutoa huduma.

"Kwa sababu ukiwa huna faida ina maana wewe unakwenda siku mbili, tatu [halafu] baada ya miaka mingapi! Unakuwa umeondoka.

Kwa mantiki hiyo, SELF Microfinance Fund inajivunia kujiendesha kwa faida, lakini kubwa zaidi ambalo pia nao huwa wanapimwa ni kuona je imkopo hiyo inawafikia kina nani?.

Ndani ya kipindi hicho, imeweza kuwafikia wateja 183,981 na kati ya hao 97,000 ni kundi la wanawake na 86,000 ni wanaume.

Pamoja na hilo, imefanikiwa katika sehemu ya pili ya jukumu lao ambalo ni kukopesha na kujenga uwezo wa taasisi ndogo za huduma za fedha hili nalo tumelifanya.

"Katika kipindi hiki, tumeweza kujenga uwezo wa taasisi zipatazo 549 tuliweza kutoa ushauri mbalimbali, kukaa nazo lakini wakati mwingine kusaidia jinsi gani wanaweza kujiendesha.

"Nafikiri wote tunatambua huduma hizi za fedha bado ni eneo ambalo tunatakiwa sana tujikite hasa katika kutoa elimu," amesema Santieli.

Eneo jingine walilofanikiwa ni kutengeneza ajira, akibainisha zaidi "Sisi tunatoa mikopo kwa taasisi ambazo zinaenda kukopesha pia kwa wajasiriamali.

"Wale wajasiriamali ambao tunawapa hizi fedha wanajiajiri lakini pia wanatoa fursa [kuna] wengine wanafanya [kazi zao] wenyewe, wengine wanakuwa na biashara kubwa na wanaajiri wengine".

Ameongeza "Tumetengeneza ajira 183,000 na haya ni mafanikio kwa nchi yetu, kwa sababu kama nchi/ Serikali haiwezi kutoa ajira kwa kila mmoja.

"Lakini kila mmoja kwa eneo lake anaweza kuona namna gani anaweza kujiajiri na kujikimu kama Mtanzania.

"Tumeanzisha pia mikopo kwa ajili ya nishati safi ya kupikia, ni agenda ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi tuliichukua kuona tunafanyaje kuunga mkono juhudi hizi.

"Tuna imani mikopo hii ikiwafikia wengine wataweza kulinda mazingira, mafanikio mengine ni kwenye kutoa elimu ya fedha," amebainisha Santieli.

UWEZESHAJI: TZS BILIONI 300 WATU 200,000 KUNUFAIKA - MFUKO WA SELF

Kiasi cha takriban TZS 300 Bil. kitatumika kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kupitia mikopo nafuu inayotolewa na SELF Microfinance.

Fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kipindi cha miaka mitano ambacho kinaanzia mwaka 2025 hadi mwaka 2030.

Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona ameweka wazi, katika mkutano wake na waandishi wa habari pamoja na wahariri wa vyombo vya habari, Dar es Salaam.

Ni katika mkutano ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ili taasisi zilizopo chini yake ziweze kueleza Umma wa Tanzania juu ya majukumu yao na hatua zilizofikiwa pia.

"SELF Microfinance Fund inayo mipango iliyojiwekea kwa miaka mitano ijayo iwe imefikia wapi katika kutimiza majukumu yake kwa Tanzania.

"Tunasema ni vizuri zaidi na tumejipanga kuwafikia wengi sana ambao wanahitaji huduma za fedha," amesema.

Amebainisha mikopo ya TZS 300 Bil. wataitoa kwa wananchi pia wanakusudia kuwa na uwezo wa kufika mbali zaidi katika kipindi hicho kufikisha huduma zake.

Amesisitiza wataimarisha na kupanua zaidi mtandao wao kutoka matawi 12 hadi 22 pamoja na eneo la mifumo yake ya ki-digitali.

"Tunataka kuongeza wanufaika, wengi zaidi angalau kufikia watu 200,000, tumeweka mikakati mizuri, tutaenda kwa 'stage' mbalimbali tutafika huko.

"Tumejipanga kuongeza ufanisi na hapa kwenye ufanisi tunataka zaidi tuone jinsi gani tutatengeneza mifumo yetu itumie teknolojia.

"... na ukiangalia kwenye dira ambayo imezinduliwa ya 2050, ukienda eneo la fedha, utaona kubwa moja ambalo tumeagizwa ni kuhakikisha tunatoa huduma zetu kwa kutumia teknolojia.

"Tukasema kweli sasa nchi ni kubwa ukisema usitumie teknolojia maana yake kuna watu hutawafikia.

"Tumejipanga kuboresha mifumo yetu ya ki-utendaji tutumie teknolojia twende mbali zaidi," amesisitiza na kuongeza,

"Kingine [ni] kuhakikisha taasisi inakuwa endelevu, kama hatujajipanga vizuri na haina misingi imara ya kuwa endelevu maana yake huduma zetu zitasita.

"Kubwa ni kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma bora zaidi, tutaangalia tena upya huduma na bidhaa ambazo tunatoa ili kuendana na wateja wanavyojhitaji," amesema.

Santieli amesema wanaendelea pia kufanya maboresho ili mwisho wa siku wawe wametoa mchango mkubwa kwa Taifa.

"Ofisi ya Msajili wa Hazina, amekuwa karibu na sisi kila wakati wametaka kuona kitu gani tunafanya je tufanyeje!.

"Tumepata ushauri na mpaka hapa tulipo ni kwa sababu ya huduma tuliyopata Ofisi ya Msajili wa Hazina," amesema.

Amesema pia kuna taasisi ambazo wanashirikiana nazo ili kusaidia kupunguza hatari inayoweza kutokea katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Hii ni biashara kuna wanaotusaidia kupunguza zile hatari.kuna wanaotupa huduma za udhamini kwa wateka wetu ili wasiweze kutetereka.

Amesisitiza wanawashukuru pia wateja wao, wamekuwa wazuri na wamechagua huduma kutoka kwetu.

"Wanaotoa huduma za fedha ni wengi sana. Lakini mpaka mtu akajipanga akaja kwetu akakopa,

"., ametuamini [na sisi] tunaamini wataendelea kubaki na tutaendelea kupata wateja wengine wazuri," amesema.

Santieli amewashukuru wahariri na waandishi wa habari kwa kuendelea kuelimisha jamii kuhusu taasisi hiyo na majukumu yake kwa ufasaha.

"Eneo la elimu, ninyi ni washirika wetu wa karibu tunataka twende pamoja.

"Tunawakaribisha kuendelea kushirikiana nasi kutangaza shughuli zetu tunazofanya," ametoa rai.

AFYA & MAZINGIRA: MIKOPO NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUWAFIKIA WENGI - MATTABA

Nishati safi ya kupikia ni agenda mahusus kwa Tanzania, inayolenga kuunganisha nguvu za pamoja katika kukabili uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Ukataji miti holela ni kati ya mambo yanayochangia uharibifu wa mazingira na kitendo hicho huathiri mifumo ya hali ya hewa na hata afya ya binadamu.

SELF Microfinance Fund imeamua kuingia katika juhudi za kusaidia nchi katika mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira na kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona amesema mfuko umeanzisha mkopo wa nishati safi ya kupikia.
Santieli amesema hayo alipozungumza mbele ya waandishi wa habari na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.
Kikao hicho huandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina mahususi kwa ajili ya taasisi zilizo chini yake kueleza Watanzania majukumu yao, mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo.

"Tunataka kuongeza wigo wa huduma kwa wananchi wengi zaidi. Mikopo ya nishati safi itasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ndani ya jamii.
"Hii itasaidia kulinda afya za wananchi lakini pia kusaidia kulinda mazingira yetu kwa ujumla," amesema.

Amesisitiza "Hii ni agenda ya Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi SELF Microfinance Fund tuliona tusibaki nyuma katika utekelezaji, kusaidia Taifa".

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara na Masoko wa Mfuko wa SELF Petro Mattaba amesema tangu kuanzisha mpango wa mikopo kwa nishati safi tayari wafanyabiashara zaidi ya 100 wamefikiwa.

Wafanyabiashara hao ni wale ambao wanajihusisha na uuzaji wa mitungi ya gesi na kwamba ni wale walio ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mkoa wa Dar es Salaam ni 'jicho' la Tanzania ukiwa hasa ndiyo kitovu cha sekta ya biashara.

Lakini, kulingana na takwimu za Ofisi ya Mkoa huo bado una kiwango kikubwa cha matumizi ya nishati chafu ya kupikia.
Mkoa wa Dar es Salaam peke yake unafanya matumizi ya zaidi ya 68% ya mkaa unaozalishwa katika maeneo mengine nchini, ni suala ambalo linahatarisha mazingira.
Mattaba amebainisha tayari "Kampuni zinazosambaza nishati safi ya kupikia hapa Dar es Salaam [tumezifikia].
"Tumeanza mwaka huu mikopo [ya nishati safi ya kupikia, kwa] kiasi cha TZS 100 Mil".
Wanufaika ambao wamechangamkia zaidi mikopo hiyo ni wakina mama na sasa kwa kiasi kikubwa [wao] ndiyo watumiaji wakubwa wa majiko ya nishati safi ya kupikia.

ELIMU DUNI: KUHUSU FEDHA, KIKWAZO KWA WAJASIRIAMALI KUKUA KI-UCHUMI

Ukosefu elimu ya fedha ni kikwazo kinachokwamisha wajasiriamali wengi hasa wadogo ndani ya jamii kiasi cha kushindwa kuendelea ki-biashara hatimaye kukua ki-uchumi.

Ni changamoto inayohitaji nguvu ya pamoja kuhakikisha elimu sahihi inawafikia watu wengi zaidi ili waweze kukomboka ki-uchumi na kuondokana na umaskini.

SELF Microfinance Fund imekuwa ikiwa elimu wananchi kwenye majumuiko mbalimbali kwa mfano nanenane, sabasaba, makongamano na kupitia vyombo vya habari.

Amesema Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona alipozungumza na waandishi wa habari pamoja na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari, Dar es Salaam.

Santieli ameongeza "[Hili la elimu] ni jukumu pana ambalo tunatakiwa tuendelee kulifanya kwa sababu tumegundua elimu ya fedha bado inahitajika kwa wengi, bado haijawafikia.

Amesema pamoja na hilo, zipo changamoto nyingine kadhaa wanazokabiliana nazo katika utendaji kazi wao.

"Changamoto ni kawaida kwa maisha ya binadamu hata ngazi ya familia zipo, kuna mafanikio lakini kuna wakati unapitia changamoto.

"[SELF Microfinance Fund] changamoto tumeziweka 'ma-group' matatu, kwanza wananchi wengi bado hawana elimu ya fedha," ametaja.

Kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya fedha, anabainisha "Unakuta mtu amekuja kuomba mkpo na hajafanya vizuri hata tathmini ya kitu anachoenda kufanya.

"Unajikuta anaweza kupata fedha lakini jinsi ya kuzitumia zitaleta matokeo hasi kwa vile hajapata elimu [kwamba] hivi nikipata fedha kipi

kitatangulia.

"[Mtu] anawaza nikaombe mkopo lakini kuhakikisha vizuri tathmini ya kitu anachotaka kuwekeza [hajafanya].

Hivyo SELF Microfinance Fund huwa wanashauri mtu kabla hajakopa afanye tathmini ya kina zile fedha[anazoomba.

"Kabla hazijaja utafanya nini? Lakini siyo fedha zikija ndiyo uanze kufikiria utaona [vitu] vingine [ambavyo] havikuwapo unafanyia kazi.

"Kwa mfano nyumbani hakupo vizuri unaenda kunua funichers, [mwisho] unakuta fedha hazitoshi kufanya maboresho ya mradi wako.

Changamoto nyingine ambayo SELF Microfinance Fund imekuwa ikikumbana nayo, anasema ni hulka ya baadhi ya watu ambao hukopa lakini hawaamini katika kulipa mikopo yao.

Amefafanua "[Mtu] anajua anakuja kuomba mkopo, lakini hajajipanga kulipa mkopo [hii] inaleta shida katika biashara hizi [za kukopesha] ile hulka.

"Ukishindwa [kulipa mkopo wako] utaanza kufuatiliwa na ukifuatiliwa lazima kuna vitu vitakuwa havijakaa sawa.

"Hata kwenye jamii mnaona, ukianza kufuatiliwa utaona wengine [wanaokufuata] wanafanya vitu visivyo vya kibinadamu.

"Lakini ni vizuri ukienda kukopa ujipange vizuri na ujue lazima ulipe mkopo," amesema na kusisitiza zaidi,

"Ukijenga hiyo hulka [ya kukopa] na ukalipa mkopo ili hata mtu akija kugonga hodi nyumbani usije ukajiuliza huyu ni nani.

Changamoto nyingine iliyopo ni kuhamahama kwa wajasiriamali wadogo, akifafanua zaidi, "Wajasiriamali [wengi bado] hawapo katika eneo rasmi.

"Unakuta wamepata tatizo wameondoka na ndiyo maana tunaona Serikali inalifanyia kazi hili kwa kuandaa maeneo rasmi ya biashara ili kuwasaidia zaidi.

"Mikoa mbalimbali kuna 'machinga complex' nia ni kuweka maeneo mazuri, hata mtu akikopeshwa mna uhakika mnamkuta pale pale.

Licha ya hayo anasema wanajivunia mafanikio mbalimbali waliyoyapata ikiwamo kufikia idadi kubwa ya wateja ndani ya kipindi cha miaka 4 [2020/21 hadi Juni, 2025].

"Tumetoa mikopo ya thamani ya TZS 196.9 Bil. na kiwango cha mikopo chechefu bado hakijazidi 10%," amesema.

Kwa kipindi hicho, tumewafikia wateja 183,981 na kati ya hao 97,000 ni kundi la wanawake na 86,000 ni wanaume.

Kwa kipindi hicho pia wamezijengea uwezo wa taasisi zipatazo 549 kwa kuzipa ushauri, jinsi bora ya kujiendesha.

"Tumetengeneza ajira 183,000, haya ni mafanikio kwa nchi yetu, kwa sababu kama nchi / Serikali haiwezi kutoa ajira kwa kila mmoja.

Amesema sasa wameanzisha pia mkopo wa nishati safi ya kupikia, kuunga mkono juhudi za Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kukabili uharibifu wa mazingira.

SELF MF: JINSI MIKOPO NAFUU INAVYOWANASUA WANANCHI KUTOKA JANGA LA UMASKINI

Ukihesabu kutoka mwaka 2015 hadi kufikia 2025 tayari ni miaka 10 sasa, tangu ilipoanzishwa SELF Microfinance Fund, umri ambao kama ni mtoto basi amejitambua na anazidi kusonga mbele.

Hatua muhimu ya ukuaji ambayo ina uwezo wa kumpa mzazi taswira ya mtoto wake wapi alipotoka, wapi alipo na wapi anakoelekea.

"Yupo mwanamke mmoja ambaye anajihusisha na ufugaji alianza na ng'ombe alipokuja kwetu kuomba mkopo, leo hii amepata mafanikio na ameweza kupanua biashara yake,".

Ni kauli yake Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona, anasema hivi sasa mwanamke ameongeza idadi ya mifugo kwa wingi ikiwamo pia mbuzi na nguruwe.

Ni Mkazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Santieli anasema mwanamke huyo ni mfano mmoja halisi wa wengi ambao wamefikiwa na mfuko huo tangu ulipoanzishwa kufikia leo.

Ndani ya SELF Microfinance Fund yapo mengi tangu kuanzishwa kwake, ukipewa jukumu la kuhakikisha unasaidia kuwakwamua wananchi hasa wa hali ya chini kutoka janga la umaskini.

Unayo haki ya kuyajua na



makala haya maalum yatakueleza namna taasisi hii iliyo chini ya Wizara ya Fedha inavyofanya kazi, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jukumu lake kubwa ikiwa ni kuhakikisha inawafikia wananchi hasa wajasiriamali wasio na uwezo wa dhamana za kukopa ma-benki, basi inawapa mikopo nafuu, isiyowaumiza wala 'kuwakausha damu'.

"Shughuli zetu hasa kubwa ambazo tumepewa ni kuhakikisha tunatoa mikopo na kuwapa watu fursa hizo za kwenda kujiongezea kipato,".

Santieli anasema hayo akibainisha kwa kina, "Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2015 ukiwa ni muendelezo wa 'project' ambayo ilikuwa chini ya Serikali.

"Kwa mwaka 2015 tulikuwa tunaendeleza kazi zile ambazo zilikuwa 'project' ambayo iliitwa 'small entrepreneurs loan facility'.

"Tuna dira [yetu], tunasema sisi ni taasisi ya huduma ndogo za fedha inayoongoza katika kubadilisha maisha ya watu," anasema.

Anaongeza "Tumependa dira yetu kwa sababu mara nyingi dira [huwa] zinalenga kwa maisha ya baadae.

"[Lakini] sisi tunachokifanya tunabadilisha maisha ya watu kwa [kuanzia maisha yao ya] sasa,".

Anasema pamoja na hilo, dhima kubwa ya mfuko huo ni kuhakikisha unawapa wananchi fursa ya kupata huduma ndogo za fedha.

MISINGI THABITI

Santieli anasisitiza "Tuna miongozo / misingi ambayo inatuongoza [katika kuwapa huduma wateja / wananchi. Msingi wa kwanza ni uadilifu.

Uadilifu ni jambo la muhimu mno kwa mtu yeyote anayetoa huduma ya mikopo kwa wananchi ni lazima awe nao.

Misingi mingine iliyopo ndani ya SELF Microfinance Fund ni kuhakikisha wanamuhudumia vema mteja wao.

"Sisi tunapenda sana tuzingatie wateja kwa sababu wateja ndiyo wanaotufanya sisi tuwepo, lakini pia tuna msingi wa ushirikiano, wa uwajibikaji pia msingi wa ubunifu," anabainisha.

Anasema vitu hivyo ndivyo

ambavyo vinawafanya hadi leo kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi tangu mfuko huo ulipoanzishwa na Serikali.

UTENDAJI ULIVYO

Majukumu makubwa ya mfuko huu, la kwanza ni kuhakikisha wanatoa mikopo ambayo imewekwa katika 'category' tofauti tofauti.

"Kwanza mikopo midogo kabisa kwa watu binafsi. Lakini sisi pia tunatoa mikopo kwa taasisi ambazo zimesajiliwa na zinafanya kazi.

"Kwa hiyo hilo ni jukumu letu la kwanza kabisa," anabainisha na kuongeza "Jukumu la pili ni kuhakikisha kwamba katika jamii tunazitambua fursa zilizopo.

"Lakini tukishazitambua tunatakiwa kutoa elimu na hiyo elimu tunatakiwa kuwapa wafanyabiashara wale wadogo wadogo, pia zile taasisi ambazo tunazipa mikopo," anabainisha.

Anataja jukumu la tatu ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo ambao wanapata hiyo mikopo kwenda kufanya kazi na kujiajiri ili Taifa lipate tija.

"Tunazo huduma mbalimbali ambazo tunazitoa ...mikopo ya aina mbalimbali kwa wajasiriamali pia [mikopo] kwa taasisi.

"Ni [zile] zilizosajiliwa kisheria kutoa mikopo ni ambazo zinasajiliwa chini ya Benki ya Tanzania [BoT].

MFANO HALISI

Anasema ipo taasisi moja Jijini Dodoma ambayo inatoa mikopo midogo midogo, kwa miaka minne sasa wamekuwa wakiwapa huduma.

"Mwanzo [mmiliki] alipokuja alikopa chini ya TZS 100 Mil, sasa ameenda mpaka TZS 500 Mil, kitu ambacho tumekiona kwake anakopesha wanawake ambao wapo kwenye vikundi vidogo vidogo.

"Ukienda utaona ni wanawake ambao hawana dhamana hawawezi kwenda benki wakapata fedha ila kwa taasisi ile wanaweza wanadhamiana kwenye vikundi wanapata fedha.

Anasema mteja wao huyo ameweza kuwafikia wanawake 4,800, "Ni watu wa hali ya chini kabisa.

"..., taasisi hiyo sasa imefungua tawi lingine Iringa, inaonesha imefikia vizuri mikopo tunayotoa imeweza kusaidia jamii na sasa inaenda mkoa jirani.

"[Sisi] imetutia moyo na tumefarijika na kwa vile tuna wateja wengi wa aina hiyo tumepiga hatua.

"Hiyo ofisini wanakaa chini kabisa, wanarejesha fedha zao wanakusanya na kupeleka benki kwa uaminifu kabisa.

Anadokeza zaidi, "Pia tuna saccos ambazo zinasajiliwa, zote hizi tunaweza kuzipa mikopo [na] tuna mikopo ya kwenda kwa mtu mmoja mmoja.

"Kwa mfano mjasiriamali au mkulima naye anahitaji mtaji kwa ajili ya kilimo anaweza pia watumishi ambao wapo katika Serikali wanahitaji mikopo [tunawapatia].

SELF Microfinance Fund ina huduma nyingine ambayo ni bima mbalimbali akifafanua zaidi "Mwanzoni tulikuwa na mikopo na suala la kujenga uwezo [elimu ya fedha].

"Lakini baadae tuliona mikopo tunayoitoa iweze kulindwa sasa ili iweze kulindwa kuna huduma mbalimbali za bima, lengo kuhakikisha tunailinda ile mikopo tunayotoa," anasema.

MTANDAO WA HUDUMA

SELF Microfinance Fund unatoa huduma kwa nchi nzima lakini tangu umeanzishwa hadi kufikia sasa umeweza kuanzisha matawi 12.

"Lakini jinsi tulivyojipanga kila tawi linakuwa na mikoa ambayo inatoa huduma. Nia yetu baadae ni kufungua matawi mengi zaidi, tutajikuta baada ya muda tutakwenda nchi nzima," anasisitiza.

Mfuko huo una tawi la Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, Mtwara, Dodoma, Tanga, Zanzibar, Kahama, Geita, Mwanza, Iringa, Mbeya.

Kwa matawi hayo wamewafikia wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mtwara, Lindi, Tanga, Dodoma, Singida, Unguja na Pemba, Sinyanga, Tabora, Katavi, Geita, Kagera pamoja na Kigoma.

Mikoa mingine ni Mwanza, Simiyu, Mara, Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya Songwe na Rukwa.

"Utaona ni mtandao tumeujenga kwa sasa na kama nilivyosema nia yetu ni kuhakikisha kila mahala tunafika," anasema Santaeli.

VIWANGO MIKOPO

Santieli anabainisha kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia Juni, 2025 wametoa mikopo ya thamani ya TZS 196.9 Bil.

Anasema kwa kipindi hicho kiwango cha mikopo chechefu wameweza kuhakikisha hakizidi 10% hadi sasa bado ni 8% tu.

"Hii inaonesha nini? [ni] kwamba hii mikopo ambayo tunaitoa inarudi kwa hiyo ndiyo maana kama ni mtaji wa Serikali unaweza kuzunguka na mwishoni tukazalisha zaidi.

"Katika vipindi vyote tangu 2020/21 hadi sasa tunajiendesha kwa faida. Hii kwetu sisi ni

fahari. Tunawafikia wananchi na tunajiendesha kwa faida.

"Tukiwa na faida inaonesha nini?... [ni] kwamba tutaendelea kuwepo na kutoa huduma," anasema.

WIGO MPANA

Kwa kipindi hicho, wameweza kuwafikia wateja 183,981 na kati ya hao 97,000 ni kundi la wanawake na 86,000 ni wanaume.

Maana yake ni kwamba huduma zetu zinawafikia watanzania katika maeneo yote haswa wanawake lakini pia wanaume kwa hiyo hakuna ambaye ameachwa nyuma.

Kwa kipindi hicho pia wamezijengea uwezo wa taasisi zipatazo 549 kwa kuzipa ushauri, jinsi bora ya kujiendesha.

FURSA AJIRA

Ni eneo jingine walilofanikiwa, kutengeneza ajira, akibainisha zaidi "Sisi tunatoa mikopo kwa taasisi ambazo zinaenda kukopesha pia kwa wajasiriamali.

Anasema watu wamejiajiri na wengine wameajiri wenzao wengi kwa kuanzisha biashara mbalimbali.

Anabainisha "Tumetengeneza ajira 183,000, haya ni mafanikio kwa nchi yetu, kwa sababu kama nchi / Serikali haiwezi kutoa ajira kwa kila mmoja.

"Lakini kila mmoja kwa eneo lake anaweza kuona namna gani anaweza kujiajiri na kujikimu kama Mtanzania.

Anasema sasa wameanzisha pia mkopo wa nishati safi ya kupikia, kuunga mkono juhudi za Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kukabili uharibifu wa mazingira.

NGUZO YA ELIMU

Anasema elimu ya fedha hutolewa kwa wananchi ikiwamo kwenye majumuiko mbalimbali kwa mfano nanenane, sabasaba, makongamano na katika vyombo vya habari.

"[Hili] ni jukumu pana ambalo tunatakiwa tuendelee kulinfanya kwa sababu tumegundua elimu ya fedha bado inahitajika kwa wengi, bado haijawafikia.

Anasema licha ya mafanikio wanayojivunia, zipo changamoto kadhaa wanazokabiliana nazo katika utendaji kazi wao.

Anataja mojawapo ni suala la elimu duni ya masuala ya biashara, uchumi na fedha kwa wananchi.

"Unakuta mtu amekuja kuomba mkpo na hajafanya vizuri hata tahmini ya kitu anachoenda kufanya.

"Unajikuta anaweza kupata fedha lakini jinsi ya kuzitumia zitaleta matokeo hasi kwa vile hajapata elimu [kwamba] hivi nikipata fedha kipi kitatangulia," anatoa mfano.

Anataja changamoto nyingine ni hulka ya baadhi ya watu ambao hukopa lakini hawaamini katika kulipa mikopo yao.

Anafafanua "[Mtu] anajua anakuja kuomba mkopo, lakini hajajipanga kulipa mkopo [hii] inaleta shida katika biashara hizi [za kukopesha].

Changamoto nyingine waliyoiona ni kuhama-hama kwa wajasiriamali wadogo, akifafanua zaidi, "Wajasiriamali [wengi bado] hawapo katika eneo rasmi.

"Unakuta wamepata tatizo, wameondolewa inaleta shida inapofika kurejesha. Naamini Serikali yetu inafanyika kazi.

"Mikoa mbalimbali kuna 'machinga complex' nia ni kuweka maeneo mazuri, hata mtu akikopeshwa mna uhakika mnamkuta pale pale.

MIAKA IJAYO

SELF Microfinance Fund inayo mipango iliyojiwekea kwa miaka mitano ijayo iwe imefikia wapi katika kutimiza majukumu yake kwa Tanzania.

"Tunasema ni vizuri zaidi na tumejipanga kuwafikia wengi sana ambao wanahitaji huduma za fedha," anasema.

Anasema wamepanga kutoa mikopo zaidi na kiasi cha TZS 300 Bil. zitatumika ambapo zitawafikia wanufaika zaidi ya 200,000.

Pia wana malengo ya kufungua matawi zaidi kutoka 12 ya sasa hadi kufikia 22 nchi nzima.

Anaongeza "Ukiangalia kwenye dira ambayo imezinduliwa ya 2050, ukienda eneo la fedha, utaona kubwa moja ambalo tumeagizwa ni kuhakikisha tunatoa huduma zetu kwa kutumia teknolojia.

"Tukasema kweli sasa nchi ni kubwa ukisema usitumie teknolojia maana yake kuna watu hutawafikia.

"Tumejipanga kuboresha mifumo yetu ya ki-utendaji tutumie teknolojia twende mbali zaidi.

Anasisitiza "Kingine [ni] kuhakikisha taasisi inakuwa endelevu, kama hatujajipanga vizuri na haina misingi imara ya kuwa endelevu maana yake huduma zetu zitasita.

"Kubwa ni kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma bora zaidi, tutaangalia tena upya huduma na bidhaa ambazo tunatoa ili kuendana na wateja wanavyojhitaji.

"Tutaendelea kufanya maboresho ili mwisho wa siku tuwe na mchango mkubwa kwa Taifa. Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia tunaishukuru kwa kuiwezesha taasisi hiyo.

UTEKELEZAJI DIRA YA TAIFA 2050 TUTATUMIA VIPAUMBELE VINANE-MFUKO WA SELF

Unaundwa mkakati maalum utakaosaidia kuimarisha huduma za utoaji mikopo nafuu kwa wananchi hasa wajasiriamali wadogo ili wakuze mitaji yao na kukua ki-uchumi, nchini.

Mfuko wa SELF tayari Bodi imeainisha vipaumbele vinane vya utekelezaji vitakavyoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 – 2050.

Hatua ambayo inalenga kuimarisha huduma zinazotolewa na Mfuko huo ulio chini ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha, ulioanzishwa mwaka 2015.

Mwenyekiti wa Bodi Paul Sangawe amezungumza kwa mara ya kwanza na waandishi wa habari - Arusha, tangu alipoteuliwa awamu ya pili na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuiongoza.

"Ni muda mwafaka wa kila taasisi kujipanga vema kuona namna gani itaweka mipango yake ili iendane na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050," amesema.

Amesema kwa uzinduzi wa dira ile tafsiri yake mojawapo ni pamoja na mashirika, taasisi za umma kujipanga upya kwa kuzingatia malengo na vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika dira.

"Kwa hiyo pamoja na mafanikio ambayo [SELF] tumepata ... huu ndiyo muda wa kujipanga, kufanya jitihada [zaidi] ili kuhakikisha mfuko unaendelea kuhudumia wananchi kwa ufanisi".

Ameongeza "Lakini pia vile vile, kufikia malengo na vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika dira.

Amebainisha vipaumbele watakavyosimamia ni ufunguzi wa matawi mapya, uelimishaji jamii, ongezeko la mtaji pamoja na uimara wa taasisi hiyo.

Pia watafanya mapitio ya viwango vya riba zake ziwe rafiki zaidi kwa wananchi, kuongeza gawio kwa Serikali na kuimarisha ushirikiano wa wadau.

Mfuko wa SELF umedhamiria kuimarisha taasisi kupitia ushirikiano wa wafanyakazi na wateja na kuwa na Mpango Mkakati wa Muda Mrefu.

Mpango huo utazingatia maeneo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa na yatakayoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Muda Mrefu [LTPP] na mipango ya kimataifa.

"Huduma za ki-fedha ni mojawapo ya kichocheo muhimu cha mageuzi ya ki-uchumi Tanzania kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 – 2050," amesisitiza.

Dira ya Taifa ilizinduliwa na Rais Dkt. Samia Julai 17, 2025 Mkoani Dodoma, inalenga kuijenga Tanzania ya baadae inayojitegemea ubunifu wa ki-digitali, ustawi wa wananchi na ujumuishi wa ki-fedha kwa wote.

Awali Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa SELF Santieli Yona amesema jukumu kubwa la kwanza walilonalo ni kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kuinuka ki-uchumi.

Amesema pia wanalo jukumu la kutoa mikopo kwa taasisi za fedha ambazo zinalenga kutoa huduma za ki-fedha kwa wananchi katika ngazi ya chini kabisa ya jamii.

"Tuna jukumu kubwa la kujenga uwezo wa wajasiriamali ki-biashara, tangu tumeanza 2015 hadi sasa, tumefanikiwa kutoa mikopo zaidi ya TZS 397 Bil," amesema.

Ameongeza "Wananchi 183,381 wamenufaika na kati ya hao 53% ni kundi la wanawake,".

TUNAJIVUNIA MAFANIKIO, TUTAONGEZA KASI ZAIDI MIAKA 5 IJAYO -SANTIELI

Hatua za mafanikio ambazo zimepatikana kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mipango yake [2021 – 2025], SELF Microfinance Fund inajivunia.

Hata hivyo, sasa unaongeza uwezo wake kwa kuweka mikakati madhubuti itakayochochea kasi zaidi ya huduma zake, kuwafikia wananchi/wajasiriamali wengi nchini.

Ndani ya kipindi hicho Mfuko umeweza kuongeza mtaji wake kutoa TZS Bil. 58.47 hadi kufikia TZS 59 Bil.

Umehudumia wananchi ambao wengi ni wajasiriamali wadogo kupata mikopo nafuu na kukuza mitaji ya biashara zao, kujikomboa ki-uchumi.

Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund Santieli Yona amesema hayo alipozungumza mbele ya waandishi wa habari, akimkaribisha Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko huo Paul Sangawe.

Pamoja na mkutano huo na waandishi wa habari, Sangawe aliongoza pia kikao cha kwanza na wajumbe wenzake wa bodi hiyo.

"Hiki ni kikao cha kueleza SELF Microfinance tulipotoka, tulipo na tunapoelekea," amesema CEO Santieli.

Amebainisha Mfuko huo una jukumu kubwa kwanza kutoa mikopo nafuu kwa wajasiriamali pia kutoa mikopo kwa taasisi za fedha zinazolenga kutoa huduma hiyo ngazi ya chini kwa jamii.

Amebainisha "Kwa kipindi cha 2021 hadi 2025 tumeweza kutoa mikopo ya TZS 199.9 Bil. na wananchi 183,381 wamenufaika,".

Santieli amesema wana jukumu kubwa la kuhakikisha wanawajengea uwezo wajasiriamali ki-biashara.

"Tangu tumeanza 2015 hadi sasa, tumefanikiwa kutoa mikopo zaidi ya TZS 397 Bil. tumewafikia wanufaika 183,381 na 53% ni wakina mama," amesema.

Amesema wanatoa huduma hiyo ya mikopo nafuu kwa kwa watu mbalimbali moja wamejikita kwenye biashara, kilimo pamoja na taasisi hizo zinazopesha.

"Tumejipanga vizuri, kuhakikisha tunafikia malengo yetu na malengo ya Serikali," amesisitiza.

Mwenyekiti wa Bodi Paul Sangawe amesema 'kiu' yake kubwa ni kuona wanafikia malengo wanayojiwekea, malengo ya Kitaifa na Kimataifa pia.

"Mtaji wa mfuko umeongezeka, kukua kwa mtaji ni pamoja na uwezo wa mfuko kuweza kutekeleza majukumu ya mfuko ambayo tumepewa," amesema.

Ameongeza "Utoaji wa mkopo zaidi ya TZS 199.9 Bil. hizi ni fedha nyingi ukiangalia kwa biashara kubwa kubwa unaweza kusema fedha hizi si nyingi sana.

"Lakini kwa wafanyabiashara ndogo ndogo fedha hizi ni nyingi sana. Ukizigawa ambazo zinaweza zikabadilisha maisha ya wananchi wngi kujiendeleza katika shughuli za uchumi na kuongeza kipato.

"Hili ni jukumu mojawapo ambalo tumepewa, tungependa kuongeza wanufaika zaidi, matawi pia ili tusogeze huduma zetu karibu zaidi na wananchi," amesema.

Mfuko huo unatoa huduma nchi nzima, hata hivyo kwa sasa una matawi yake Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kahama, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Tanga pamoja na Zanzibar.

SHUHUDA ZA WANUFAIKA

TEDDY MTINANGI: MTAJI WANGU UMEKUA, NIMETOKA 'TREI' 12 HADI 30 KWA SIKU

Ni mfano hai wa namna uwezeshaji ki-fedha unavyoweza kubadili maisha, Teddy Mtinangi kabla ya kukutana na SELF Microfinance Fund, alikuwa akifuga kuku 400 na kukusanya 'trei' 12 za mayai kwa siku. Mapato yake kwa mwezi yalikuwa yakipanda na kushuka kati ya TZS 900,000 hadi milioni moja hali iliyomfanya wakati mwingine kushindwa kusonga mbele.

"Nilianza kwa kukopa mikopo ya kikundi cha watu watano na kuweka kuku wa nyama, lakini changamoto zilikuwa kubwa, nilipata hasara mara nyingi. Kuna wenzetu walishindwa kurejesha, tukajikuta tunabeba mzigo wao kwa kujichanga na kuwalipia, nilikata tamaa," anasema Teddy.

Baadae alikutana na SELF Microfinance Fund na alipata nafasi ya kuchukua mkopo binafsi, fedha hizo aliziweka moja kwa moja kwenye mradi wake wa ufugaji na matokeo hayakuchukua muda

mrefu kuonekana. Sasa ana kuku 1,200 na anakusanya zaidi ya 'trei' 30 kwa siku.

"Kwa sasa nauza takribani 'trei' 30 kila siku na mapato yangu kwa mwezi yanafika kati ya TZS 3 Mil. hadi 4 Mil. ikiwa soko lipo vizuri. Ninamudu kuwasomesha watoto wangu kwenye shule bora, wengine wako vyuoni sasa, maisha yanasonga mbele bila shida," anasema kwa tabasamu.

Teddy ana ndoto ya kukuza mradi wake zaidi na kufuga hadi kuku 3,000. Anao ushauri maalum kwa wajasiriamali hasa wanawake,

"Wasiogope mikopo. Lakini mkopo ukichukuliwa, lazima uwe na mpango wa kweli. Usitumie fedha kwenye mambo ambayo hayatazalisha. Ukiwa na nidhamu, mkopo unakua baraka," anasisitiza.

JOHNPHASE MOLLEL-NINA NDOTO YA KUWA MFUGAJI MKUBWA, SELF MF IMENIINUA

Ni mfugaji wa ng'ombe wa maziwa aliyeanza na mtaji mdogo mno, akivuna maziwa kidogo na kupata kipato kidogo, sasa anaishukuru SELF MF. kwa kumpa mkopo nafuu uliomuwezesha kuongeza ng'ombe wawili ndani ya zizi.

"Kwa ng'ombe nilionunua na SELF MF. sasa napata faida kubwa kwani ng'ombe mmoja hutoa lita 30 kwa siku (yaani lita 15 asubuhi na 15 jioni)." Anasema awali kabla ya hapo kwa ng'ombe aliokuwa nao alikuwa akipata TZS 50,000 hadi 200,000 tu kwa mwezi.

Lakini baada ya kuungwa mkono na SELF MF. kipato chake kimeongezeka kwa kiwango kikubwa, kiasi cha kumpa hamasa ya kupanua zaidi shughuli zake. "Nategemea baada ya miaka mitatu nitakuwa na ng'ombe 20 wa maziwa," anasema.

Anasema leo hii yeye si mfugaji tu bali pia amekuwa mwalimu wa wenzake. "Wafugaji wengine wanashangazwa kila mara naleta ng'ombe mpya, basi huwa nawaelekeza ilipo SELF MF. ili nao wakakope. Pia nawaelimisha juu ya namna ya kutumia mkopo kwa ufanisi, ili usije ukakopa ukautumia vibaya."

Johnphase anasisitiza kuwa SELF MF. inakopesha bila ubaguzi kwa watu wa jinsi zote (iwe mwanamume au mwanamke), mradi una mpango kamilifu wa kile ambacho unataka kwenda kutekeleza kwa mkopo utakaochukua.

Anahimiza jamii, "Ukikopa kwa ajili ya mradi, utapata matunda. Lakini ukikopa ukaongeza mke au ukaenda kwenye meza ndefu (pombe), utapoteza kila kitu." Anasema moja ya thamani kubwa aliyokutana nayo SELF MF. ni huduma rafiki kutoka kwa watumishi wake.

"Sijawahi kuombwa rushwa, sijawahi kuelezwa kwamba ili upate mkopo lazima utoe kitu. Watumishi wa SELF MF. hawana urasimu, wananisaidia kwa ushirikiano mkubwa. Ndiyo maana natamani kila mtu akakope huko, akafaidi yale niliyofaidi mimi".

TEDDY MCHOME-BIDHAA ZANGU ZA ASILI SASA ZIMEPATA SOKO HADI NJE YA NCHI

Ndani ya jiji la Arusha, jina la Teddyjoo Naturals linakua kwa kasi, ni biashara inayozalisha bidhaa za nywele na ngozi zinazotengenezwa kwa malighafi za mimea asilia bila kemikali hatarishi.

Alipoanza safari yake hiyo ya ujasiriamali, Teddy Mchome alikuwa na mtaji mdogo na wateja wachache ndani ya jiji hilo lenye hadhi ya utalii nchini Tanzania. Uwezo wa kuzalisha bidhaa yake ulikuwa mdogo kufikia malengo makubwa aliyokuwa nayo kwa siku zijazo.

Lakini baada ya kukutana na SELF Microfinance Fund, mambo yakabadilika kabisa, anabainisha, “SELF MF. walitupa mkopo nafuu nikaweza kuongeza mtaji wangu. Tukazalisha bidhaa nyingi zaidi, tukafungua masoko mapya.

“Leo hii tunasafirisha hadi mikoani na hata nje ya nchi. Tumepanua huduma zetu, tuna saluni tatu Arusha na mawakala sehemu mbalimbali,” anasema Teddy. Teddyjoo Naturals pia imekuwa dira ya ajira na matumaini kwa vijana, ameweza kuwapa ajira zaidi ya 30 wakiwemo pia miongoni mwao wenye ulemavu wa kusikia.

Wanafanya kazi ya kutangaza na kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya bidhaa zetu asilia pamoja na manufaa yake. “Uaminifu ni mtaji. Wanawake tunapokopa lazima tulipe kwa wakati. Ukifanya hivyo, unajengea benki imani na utapewa mikopo mikubwa zaidi”.

“Vijana pia wasibweteke na vyeti vyao, wajiwekee malengo ya kujiajiri. Mtu anaweza kuajiri hata waliosoma zaidi yake,” anasisitiza. Mfuko wa SELF kwa Teddy haikuwa tu chanzo cha fedha, bali chachu ya kufungua milango ya ndoto kubwa zaidi, fursa mpya za ajira kwa vijana pamoja na ustawi wa afya bora.

HABARI KATIKA PICHA

Mkoani Arusha Mwenyekiti wa Bodi Paul Sangawe akiambatana na Afisa Mtendaji Mkuu wa SELF Microfinance Fund pamoja na baadhi ya wafanyakazi walifanya ziara ya kikazi kuwatembelea baadhi ya wanufaika wa mikopo nafuu inayotolewa na Mfuko. Kwa pamoja walijionea jinsi wajasiriamali walivyopiga hatua ikiwamo kukuza mitaji yao, kuongezeka mapato yao na kupanuka kwa masoko yao ndani na nje ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Bi. Jenifa C. Omolo alipokuja kutembelea Banda la Mfuko wa SELF wakati wa maonesho ya 88 Dodoma.

Wananchi wakipatiwa elimu kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Self Microfinance Fund katika maadhimisho ya nanenane - 2025 yaliyofanyika hivi karibuni.

MATANGAZO

UJUE MTANDAO WA SELF MICROFINANCE FUND

BIMA NDOGO ZA MAGARI (Third Party Insurance)	GHARAMA YA BIMA KWA MWAKA (Tsh)	BIMA KUBWA ZA MAGARI BINAFSI (Private Comprehensive Insurance)	GHARAMA YA BIMA KWA MWAKA (Tsh)
Gari ndogo ya Binafsi	118,000	Gari Binafsi - Milioni 7	295,000
Gari ndogo ya Biashara	177,000	Gari Binafsi - Milioni 10	413,000
Gari yenye Tani 0-2	177,000	Gari Binafsi - Milioni 15	619,500
Gari yenye Tani 2-5	236,000	Gari Binafsi - Milioni 20	826,000
Gari yenye Tani 5-10	295,000	Gari Binafsi - Milioni 25	1,032,500
Gari yenye Tani 10-zaidi	334,000	Gari Binafsi - Milioni 30	1,239,000
Trailer za kawaida	118,000	Gari Binafsi - Milioni 35	1,445,500

THAMANI YA NYUMBA	ADA KWA MWAKA (MIEZI 12)
30,000,000	59,000
50,000,000	88,500
100,000,000	177,000
200,000,000	354,000
300,000,000	531,000



SELF MF

"Kuwapa Watu Fursa ya Kufanya Shughuli za Uzalishaji Mali"

KARIBU UWASILIANE NASI
Namba: 0693 290 778 au 0764 905 092 info@self.go.tz www.self.go.tz Facebook SELF MF Instagram self-mf YouTube selfmicrofinance